THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

NOVEMBER 1995

021

# KISWAHILI

(Kwa watahiniwa walioko na wasioko shuleni)

MUDA: Saa 3.00

---

## MAAGIZO

1. Jibu maswali manane (8) tu, maswali MANNE kutoka Sehemu A na maswali YOTE ya Sehemu B.

2. Zingatia maagizo ya kila SEHEMU na ya kila swali.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A : FASIHI

### KIFUNGU (i) FASIHI SIMULIZI

(Jibu swali la 1 au la 2)

1. "Mabadiliko katika Fasihi Simulizi ni ya lazima na yanatokea kulingana na mabadiliko katika jamii". Jadili tamko hili kwa hoja na mifano madhubuti.

AU

2. "Ingawa methali zina busara ndani yake, lakini kuna wakati zinapotumiwa huleta hasara." Thibitisha hasara ipatikanayo kutokana na methali zifuatazo:

   (a) La kuvunda halina ubani.

   (b) Yote yang'aayo usidhani dhahabu.

   (c) Kikulacho ki-nguoni mwako.

   (d) Mvumilivu hula mbivu.

### FASIHI ANDISHI

### KIFUNGU (ii) - USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| TEUZI ZA NAFSI | - | F. Semghanga |
| MASHAIRI YA SAADANI | - | S. Kandoro |
| MASHAIRI YA CHEKACHEKA | - | T.A. Mvungi |

3. "Katika kazi nyingi za fasihi, mwandishi aliyeshikamana na jamii yake ni mtu anayetegemewa sana kwa mawaidha, mashauri na maelekezo". Chagua waandishi wawili kati ya F. Semghanga, S. Kandoro na T.A. Mvungi na jadili washairi hao walivyofikia upeo huo.

4. "Fani ni muhimu sana katika kuifanya kazi ya fasihi ikubalike kuwa kazi ya sanaa". Chagua vitabu viwili kati ya TEUZI ZA NAFSI, MASHAIRI YA KANDORO na MASHAIRI YA CHEKACHEKA ujadili vipengele muhimu vya kisanaa vinavyojenga kazi hizo.

### KIFUNGU (iii) RIWAYA/HADITHI

| | | |
|---|---|---|
| SHIDA | - | N. BALISIDYA |
| KULI | - | S.A. SHAFI |
| KUSADIKIKA | - | S. ROBERT |

5. "SHIDA, KULI na KUSADIKIKA ni vitabu vinavyotetea haki na maendeleo ya binadamu." Chagua vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa ujadili kauli ya hapo juu.

AU

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

6. Jadili jinsi gani majina ya vitabu viwili kati ya KUSADIKIKA, KULI na SHIDA yanavyosadifu maudhui ya riwaya hizo.

KIFUNGU (iv) TAMTHILIYA

HARAKATI ZA UKOMBOZI - P. MUHANDO
HAWALA YA FEDHA - A. LIHAMBA
NGOSWE - PENZI KITOVU CHA UZEMBE - E. SEMZABA

7. "Ukosefu wa Elimu ni kipingamizi kikubwa katika maendeleo ya jamii." Jadili ukweli huu kama unavyojitokeza katika tamthiliya mbili kati ya HARAKATI ZA UKOMBOZI, HAWALA YA FEDHA na NGOSWE-PENZI KITOVU CHA UZEMBE.

AU

8. Jadili matumizi ya lugha katika kufikisha ujumbe wa tamthiliya mbili kati ya HARAKATI ZA UKOMBOZI, HAWALA YA FEDHA na NGOSWE-PENZI KITOVU CHA UZEMBE.

SEHEMU B : LUGHA

9. UFAHAMU

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali:

Kimwaga: Amina sogea huku, huyo mlevi atakukanyaga. (Amina anampisha mlevi na kumkaribia Kimwaga). Watu wengine wana raha sana - mchana wameyachapa.

Amina: Watoto wanalala na njaa!

Mtu 2 : (Anayumba). Mtu chake bwana. Hela yangu nanywea gongo. Kama wewe unakunywa bia - utajaza. Kwanza bei yake utaiweza ? Eti mchana ...mchana gongo halipiti ? Nyie mabwege. Ohho-ooo hehe - hehe ... piga hayo magoma nyie. (Watu wengine wanasema lakini maneno yao hayasikiki na kufahamika)

Kiongozi: Haya jamani eee, sasa tusikilizane! Tusikilizane! (Anaongeza sauti na kupiga makofi). Tusikilizane. (Sauti zinapungua).

Mtu 1: Kiongozi mtu bwana. Ana komandi watu wanasailensi ... sema bwana mkubwa.

Kiongozi: Hatutaki hayo maelezo yako. Huu sio mkutano wa walevi. Eee, kama tulivyotangaziwa, leo tunakutana kuelezwa kuhusu janga kuu la dunia. Hapa tunaye Dakta Mbogo. Huyu kushoto kwangu ni Bwana Afya wa Mkoa, ndugu Kileo, na na ...

Mtu 2: Haya sasa tuna Mbogo, Kileo, UKIMWI unaambaa, pigeni ngoma nyie watwana!

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Kiongozi: (Kwa hasira sana anaisogelea hadhira). Walevi wa mchana mnatuharibia mkutano. Nyie walinzi, waondoeni watu hawa. Wamelewa pombe au madawa ya kulevya ? Maadui wa siasa yetu.

Mtu 2 : Mlinzi, njoo tucheze ngoma. (Anayumbayumba).

Mtu 3 : Unanikanyaga ! (Anampiga makofi na kumsukuma mbali, mlevi anaanguka na kutulia).

Kimwaga: Hii ndio dawa yao. (Mlinzi anakuja na kumburuza Mtu 2. Mlinzi mwingine anamkamata Mtu 1 na kumwondoa. Hali inatulia).

Kiongozi: Kama nilivyokuwa nasema, wale ni wauguzi Patel na Kapeche. Nafikiri ni vizuri nimkaribishe Dakta Mbogo atueleze aliyo nayo. Karibu Dakta.

Dakta Mbogo: Asante sana Kiongozi na Wananchi. Nitaeleza kwa kifupi chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI na kuenea kwake. Hatimaye wenye maswali watapata nafasi ya kuuliza na kujibiwa. UKIMWI ni ugonjwa unaodhoofisha nguvu za mwili. Vijidudu vya UKIMWI ni virusi. Kwa kitaalamu hivi vijidudu vinavyoua kinga ya mwili wa binadamu vinaitwa HIV. Virusi hivi vikiingia mwilini vinaua askari wanaolinda mwili wa binadamu. Sote tunajua askari wanaotulinda wakiuawa na sisi tuko hatarini. Mwili ukikosa walinzi au kinga basi huweza kushambuliwa na ugonjwa wowote na mgonjwa hufa. Kitu kibaya zaidi ni kwamba hadi sasa hakuna dawa ya kutibu wala kuzuia ugonjwa huu. (Anakohoa kidogo).

Sasa nizungumzie kuenea kwa ugonjwa huu. Ndugu Wananchi, katika jambo hili tunalazimika kutumia maneno ambayo kwa kawaida hayatumiki hadharani. Kwa hiyo tuvumiliane. Katika mwili wa binadamu kuna vitu vitatu vinavyoweza kuchukua vijidudu au virusi vya UKIMWI. Vitu hivyo ni damu, mbegu za kiume na maji ya ukeni. Kwa hiyo UKIMWI unaenea wakati kimojawapo kinatoka kutoka kwa mtu mwenye HIV na kuingia kwenye mtu asiye na HIV. (Anakohoa tena)

Kileo: Daktari, naona nikusaidie kumaliza. (Anainuka na Daktari anakaa). Daktari amezungumza sana ... jana tulikuwa Mjimwema, juzi Kisumu. Lazima amechoka. Kutokana na hayo yaliyoelezwa, UKIMWI huambukizwa kwa njia kuu nne: kwanza kufanya mapenzi na mtu mwenye HIV. Pili kutumia sindano, sirinji, nyembe na vifaa vingine vyenye HIV. Tatu, ni mja mzito mwenye HIV kumpa mwanawe tumboni virusi hivyo. Nne, ni mtoto kunyonya maziwa ya mama mwenye HIV. Watafiti wengine wanasema maziwa ya mama yana vitu ambavyo vinaua virusi vya UKIMWI. Mtu mwenye UKIMWI hupata homa za mara kwa mara, huhara, huumwa kichwa na kuwa dhaifu sana. Dalili hizi hazithibitishi kuwa mtu anao UKIMWI, bali hutupa shaka. Kwa hiyo baada ya kuona dalili hizi ni muhimu kwenda hospitalini haraka. (Anatulia kidogo na kushika kasha. Vijana wenye ngoma wanazipiga kwa mahadhi ya mdundiko na kuacha ghafla).

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Maswali:

(a) Kimwaga ana maana gani asemapo, "... Watu wengine wana raha sana - mchana wanayachapa." ?

(b) Virusi vya ukimwi vinafanya nini vikiingia mwilini ?

(c) Katika mwili wa mwanadamu ni vitu gani vinaweza kuchukua virusi vya ukimwi ?

(d) Taja njia nne za kuambukiza ukimwi.

(e) Ni kwa vipi matumizi ya Mtu 1 na Mtu 2 yamejenga au kuharibu mazungumzo haya ?

10. Andika ufupisho wa habari uliyoisoma katika swali la 9 kwa kutumia maneno yasiyozidi mia mbili (200).

11. Andika insha yenye maneno yasiyopungua 250 na yasiyozidi 300 juu ya mada moja kati ya zifuatazo:

(a) Ajali haina kinga

(b) Umuhimu wa elimu ya ufundi nchini

(c) Nafasi ya vijana katika maendeleo ya taifa

(d) Ajali za barabarani.

12. (a) Kwa kila sentensi onyesha Kiima na Kiarifu kwa kupigia mstari na kuandika K kwa Kiima na A kwa Kiarifu na taja aina za maneno yote kama yalivyotumika katika kila sentensi.

(i) Juma amekunywa maji machafu mno.

(ii) Waliotolewa darasani wanafunzi wenye nguo chafu.

(iii) Apendae taarab aingie sasa ukumbini.

(iv) Utoro ulimponza mwanafunzi mwaka jana.

(v) Ajali ya treni Kilosa ilitusononesha mioyo.

(b) Sahihisha sentensi zifuatazo:

(i) Samaki hizi zimechina

(ii) Kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu, kwa hiyo ni budi tukitilie mkazo.

(iii) Nyinyi ote njooni hapa.

(iv) Mahakama imemtoa mtuhumiwa kutoka rumande kwa mzamana wa shilingi elfu tano.

---

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner